


Bibilia ya watoto

Inawalettea

Mkulima na
Mbegu



Kimeandikwa na: Edward Hughes
Kimeorodheshwa na: M. Maillot; Lazarus
Imerekebishwa na: E. Frischbutter; Sarah S.
Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya
Alastair Paterson
Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

BFC
PO Box 3
Winnipeg, MB R3C 2G1
Canada


©2020 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.



Siku moja Yesu alifundisha
kando ya ziwa. Watu wengi
walikusanyika kumsikiliza.
Kusanyiko likawa kubwa

sana. Yesu
angefanya nini?




Yesu alipoona mashua iko karibu, akaipanda. Akawa sasa anawaona watu na wao wakaweza kumuona na kumsikia.



Yesu akaanza kuwaambia
mifano - hadithi za mambo ya
kawaida ambazo ziliwafundisha
watu kuhusu Mungu.



"Mkulima alipanda mbegu kwa kutawanya kwenye shamba lake."
Hadithi ya Yesu ilikuwa kama picha yenye maneno badala ya michoro.





Watu waliweza kuelewa picha ya mkulima
anayefanya kazi - walishaona mara
nyingi.




Baadhi ya mbegu
zilizopandwa kwa
kutawanywa zilianguka karibu
na njia. Ndege wakashuka
kwa kasi na kuzila.




Baadhi ya mbegu zikaangukia sehemu zenye mawe shambani. Zikakua upesi kuwa mimea mirefu, myembamba na dhaifu. Mara jua kali likainyausha kwa sababu haikuweza kuwa na mizizi mirefu kwenye udongo wenye kina kifupi.




Mbegu zingine zikaota
kwenye miiba. Hazikuzaa
matunda. Miiba ilisonga
mimea michanga ikazuia
kupata mwanga wa
jua na mvua.




Mbegu zilizobaki zikaangukia kwenye udongo mzuri. Baada ya muda kupita, zikawa mimea yenye afya na kuzaa nafaka nyingi mpya. Mkulima akafurahi sana.



Mwisho wa hadithi, wanafunzi wakaja kwa Yesu wakamuuliza, "Kwanini unafundisha kwa mifano?"




Yesu akasema mifano inawasaidia watu kuelewa kuhusu Mungu kama kweli wanampenda. Watu wasiompenda Mungu hawawezi kuelewa mifano.




Yesu akaiielezea mifano. Akasema
mbegu ni Neno la Mungu. Mbegu
zilizoanguka njiani ni kama mtu anayesikia

lakini
haelewi Neno
la Mungu.


Shetani
anamsahaulisha
kile alichosema
Mungu.



Baadhi ya watu wanalipokea Neno la Mungu kwa haraka. Wanafanana na mbegu iliyoangukia kwenye udongo wa mawe. Lakini mara tu mtu anapowadhihaki au kuwasumbua kwa sababu ya kumpenda Mungu, jambo la huzuni hutokea.



Watu hawahawa ambao walianza kwa furaha kumfuata Yesu wanageuka na kuacha kutii Neno la Mungu. Hawataki kulipa gharama ya kumfuata Mungu. Inasikitisha sana kwamba wanataka kuwapendeza marafiki badala ya kumpendeza Mungu!



Miiba katika huu
mfano ni kama
masumbufu
ya dunia na kupenda
fedha, tabia ambazo
zimejaa katika maisha
ya baadhi ya watu.
Wanajishughulisha
sana katika kujaribu
kupata fedha zaidi
na mambo mengine
kiasi kwamba Mungu
anakuwa nje ya
maisha
yao.



Lakini mbegu zilizoangukia kwenye udongo mzuri na kuzaa mavuno mazuri ni kama Neno la Mungu linaloingia moyoni mwa watu na kubadilisha maisha ya watu. Watu hawa wanamtumikia na kumheshimu Mungu.



Makundi ya watu hayakutaka kutawanyika. Wengi walitaka kumfuata Mungu na kumpendeza. Mifano ya Yesu iliwasaidia kuelewa jinsi ya kumtii Mungu.



Mkulima na Mbegu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Mathayo 13

“Kufafanusha maneno yako kwatia nuru.”


Zaburi 119:130





Mwisho

43



60



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

